**TAARIFA FUPI KUHUSU HALI YA HUDUMA YA MAJI**
**MKOA WA LINDI**

**JUNI 2017**

## 1. Hali ya Huduma ya Maji Vijijini

Hadi kufikia mwezi Juni, 2017 asilimia 52.3 ya wakazi waishio vijijini katika mkoa wa Lindi wanapata huduma ya majisafi na salama. Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji katika kila Wilaya kwa maeneo ya vijijini ni kama inavyoonekana kwenye **Jedwali Na. 1**. Wananchi wengi waishio vijijini hutegemea zaidi vyanzo vya maji ya mito, chemichemi zilizohifadhiwa na visima.

**Jedwali Na. 1: Hali ya upatikanaji wa huduma ya maji vijijini katika kila Wilaya**

| Na. | Halmashauri | Idadi ya Watu katika Halmashauri | Idadi ya Watu waishio vijijini | Idadi ya Watu wanaopata huduma ya maji vijijini | Vituo vya kuchotea Maji | Asilimia ya upatikanaji wa huduma ya Maji vijijini |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Kilwa DC | 190,744 | 172,142 | 99,842 | 197 | 58 |
| 2. | Lindi DC | 194,143 | 194,143 | 106,250 | 191 | 54.7 |
| 3. | Lindi MC | 78,841 | 35,699 | 19,251 | 44 | 53.9 |
| 4. | Liwale DC | 91,380 | 64,839 | 37,250 | 107 | 57 |
| 5. | Nachingwea DC | 178,464 | 153,244 | 68,960 | 99 | 45 |
| 6. | Ruangwa DC | 31,080 | 122,508 | 55,313 | 236 | 45.2 |
| **JUMLA** | | **864,652** | **742,575** | **386,866** | **874** | **52.3** |

### 1.1. Mpango wa Kuongeza Upatikanaji wa Huduma ya Maji Vijijini

### 1.2. Utekelezaji wa Miradi katika Vijiji 10 katika kila Halmashauri

Vijiji vilivyopewa kipaumbele katika kupata huduma ya maji kupitia Awamu ya Kwanza ya utekelezaji wa Programu chini ya Programu Ndogo ya Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini katika Halmashauri za mkoa wa Lindi vimeoneshwa kwenye **Jedwali Na. 2**

**Jedwali Na. 2: Vijiji Vilivyopewa Kipaumbele na Halmashauri katika kutekeleza**

| HALMASHAURI | VIJIJI VILIVYOPEWA KIPAUMBELE |
|---|---|
| Kilwa DC | Mtandi, Njinjo, Ngea, Hanga, Nanjirinji,Kandawale. Mingumbi, Kililima, Naipuli, Tingi, Mtandango na Miteja |
| Lindi DC | Rondo Mnara, Namkongo, Kiwawa, Likwaya, Hingawali, Namangale, Litipu, Nyangamara A Nyangamara B, Nahukahuka A, Nahukahuka B, Kilolombwani, |
| Lindi Manispaa | Mmukule, Nanembo, Mchochoro, Tulieni, Mitumbat7i,Mtange,Mingoyo, Mnazi mmoja, Mawasiliano, Kitunda, Kitumbikwela, Nachingwea, Likotwa, Likabuko, Kiwanjani,<br>Koleji, Likabuko, Nanjinga, Jangwani, Mkanga |
| Liwale DC | Mpigamiti, Namakololo, Mitawa, Namihu, Mbaya, Namtumbwa, Kichonda, Barikiwa, Nabuya |
| Nachingwea DC | Mkoka, Rweje, Farm 8, Lipuyu, Nampemba, Mituguru, Chiola, Kitandi, Nakalonji na Mkotokuyana |
| Ruangwa DC | Luchelegwa, Nandagala A, Nandagala B, Ng’au, Mchichili, Nahanga, Mtondo, Chikundi, Mandawa chini na Mihewe, Mbekenyera na Naunambe, Chimbila B |

Hadi kufikia mwezi Juni, 2017 jumla ya miradi 39 katika Halmashauri za Mkoa wa Lindi inatekelezwa ambapo, miradi 35 ujenzi wake umekamilika, miradi 4 ujenzi wake unaendelea kama ambavyo **Jedwali Na. 3 na Jedwali Na. 4** yanavyoonesha. Miradi yote itakapo kamilika jumla ya vijiji 71 vitapata huduma ya maji.

**Jedwali Na. 3: Miradi iliyopangwa kutekelezwa na inayotekelezwa**

| Na. | **Halmashauri** | **Miradi iliyopangwa kujengwa** | **Miradi iliyoanza kujengwa** | | **Miradi iliyokamilka** |
|---|---|---|---|---|---|
| | | **Idadi** | **Idadi** | **Vijiji** | **Idadi** |
| 1 | Kilwa DC | 10 | 7 | 12 | 7 |
| 2 | Lindi DC | 8 | 7 | 11 | 5 |
| 3 | Lindi MC | 7 | 7 | 20 | 6 |
| 4 | Liwale DC | 10 | 6 | 9 | 6 |
| 5 | Nachingwea DC | 10 | 7 | 7 | 7 |
| 6 | Ruangwa DC | 13 | 5 | 12 | 4 |
| | **Jumla** | **58** | **39** | **71** | **35** |

**Jedwali Na. 4: Jedwali linaloonesha Utekelezaji wa Miradi ya Maji kwa kila Halmashauri**

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Kilwa DC | Njinjo | 4120 | Ujenzi wa tanki la mita za ujazo 100, Mnara wa urefu wa mita 6, vituo 11 vya kuchotea Maji, Ujenzi wa nyumba 2 za kuhifadhia jenereta, Mtandao wa bomba, ufungaji wa pampu 2 (submersible pump) na jenereta 2 na mfumo wa Maji ya Mvua. | Mradi umekamilika | 100 | 460,878,880 | Unatoa Huduma |
| Kilwa DC | Nanjirinji | 4475 | Ujenzi wa tanki lenyemita za ujazo 100, Mnara wa urefu wa mita 9, vituo 15 vya kuchotea Maji, Ujenzi wa nyumba ya kuhifadhia jenereta, Mtandao wa bomba, ufungaji wa pampu 1(submersible pump) na jenereta 1 na pampu ya mkono 1 na Mfumo wa Maji ya Mvua. | Mradi umekamilika | 100 | 426,747,056 | Unatoa Huduma |
| Kilwa DC | Ngea | 268 | Ujenzi wa tanki lenye mita za ujazo 25, vituo 2 vya kuchotea Maji, Ujenzi wanyumba ya kuhifadhia jenereta, Mtandao wa bomba, ufungaji wa pampu 1(submersible pump) na jenereta 1. | Mradi umekamilika | 100 | 460,878,880 | Unatoa Huduma |
| Kilwa DC | Mtandi | 1160 | Ujenzi wa tanki lenyemita za ujazo 50, Ujenzi wa mnara wa tanki urefu wa mita 6, ujenzi wa vituo 4 vya kuchotea Maji, Ujenzi wa nyumba | Mradi umekamilika | 100 | 218,089,135 | Unatoa Huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | ya kuhifadhia jenereta, Mtandao wa bomba, ufungaji wa pampu 1(submersible pump) na jenereta 1 na ufungaji wa pampu 1 ya mkono umekamilika na ujenzi wa mfumo wa uvunaji wa maji ya Mvua. | | | | |
| Kilwa DC | Kandawale | 3200 | Ujenzi wa tanki lenye mita za ujazo 75, Ujenzi wa mnara wa tanki urefu wa mita 6, vituo 9 vya kuchotea Maji, Ujenzi wa nyumba ya kuhifadhia jenereta, Mtandao wa bomba, ufungaji wa pampu 1(submersible pump) na jenereta 1 na ufungaji wa pampu 2 za mkono na ujenzi wa mfumo wa uvunaji wa maji ya Mvua. | Mradi umekamilika | 100 | 291,795,180 | Unatoa Huduma |
| Kilwa DC | Hanga | 2300 | Uchimbaji wa visima vifupi 11 vya Ringi na ufungaji wa pampu 11 za mkono. | Mradi umekamilika | 100 | 74,000,000 | Unatoa Huduma |
| Kilwa DC | Mradi wa Maji Mingumbi-miteja | 18,120 | Ujenzi wa tanki chini 500m3,collection sump 100m3 na 50m3,tanki ya juu 150m3, Kuchimba na kulaza bomba kuu(9,896m) ,Kuchimba na kulaza bomba la kusambaza maji(61,619m), Vituo vya kuchotea maji 44(Double type), Kufunga transifoma 2 na kufunga pampu 3(pampu 1 juu ya ardhi(surface | Mradi umekamilka | 100 | 4,748,358,164.9 | Unatoa Huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | pump)), pampu 2 chini ya Kisima(Submersible pump)) Kujenga matanki ya kuvunia maji ya mvua 18 | | | | |
| Lindi DC | Mradi wa Maji Rondo Mnara | 2000 | Kujenga tanki la maji chini ya ardhi ujazo wa 100m³,kujenga tanki la maji juu ya ardhi 50m³,kujenga kibanda cha pampu, kuchimba na kulaza bomba umbali wa km 2.961, kujenga vituo 4 vya kuchotea maji, kujenga mifumo ya maji ya mvua katika kijiji cha Mnara | Mradi umekamilika | 100 | 220,737,990.37 | Hali ya huduma hairidhishi kwa sababu mitambo ya maji katika chanzo na pia katika kituo cha cha kuongeza nguvu pamoja na mabomba ya upandishaji na usambazaji wa maji katika vijiji vingine yamechakaa |
| Lindi DC | Mradi wa Maji Namkongo | 1500 | Kuchimba visima 2,kujenga kibanda cha pampu,kujenga tanki la juu 50m³,kulaza bomba na kujenga vilula 3 vya kuchotea maji | Mradi umekamilika | 100 | 133,182,765.6 | Unatoa huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Lindi DC | Mradi wa Maji Kiwawa | 500 | Kujenga na kufunga Pampu 2 za mkono na kujenga matenki 3 ya mfano ya uvunaji wa maji ya mvua | Mradi umekamilika | 100 | 44,200,000 | Visima vinatoa huduma |
| Lindi DC | Mradi wa Maji Namangale | 7000 | Kuchimba kisima, kujenga tanki la maji,kulaza bomba na kujenga vilula 16 vya kuchotea maji | Mkandarasi ameshajenga tanki la kuhifadhia Maji, amechimba mtaro na kufunga bomba kwa urefu wa mita 8,080, amejenga vilula 16 vya kuchotea maji, amejenga mifumo ya uvunaji maji ya mvua, amekamilisha kupaua na kujenga uzio katika kibanda cha mtambo na katika tanki. Amefunga pampu na Jenereta. Amemaliza kazi ya kuchimba Mtaro na ujenzi wa Birika(weir) . | 98 | Ujenzi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2017 | Ujenzi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2017 |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaik a | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Lindi DC | Mradi wa Maji Likwaya | 1000 | Kujenga tanki la juu 25m³,kulaza bomba na kujenga vilula 2 vya kuchotea maji | Mradi umekamilika | 100 | 190,071,934 | Unatoa huduma |
| Lindi DC | Mradi wa Maji wa Litipu, Nyangam ara,na Nahukahu ka | 11,000 | Kujenga matanki 2 ya maji chini ya ardhi ujazo wa 100m³ , kujenga tanki la maji chini ya ardhi 50m³, kujenga tanki la maji juu ya ardhi 25m³, kujenga tanki la maji juu ya ardhi 100m³, kujenga tanki juu ya ardhi ujazo wa 75m³, kujenga kibanda cha pampu | Bomba zote zipo eneo la kazi. Mkandarasi ameshafunga bomba urefu wa mita 13,000. Katika kijiji cha Chemichemi tanki limefunikwa na Nyumba ya Mtambo imeezekwa. Litipu- Nyumba ya mtambo inaendelea kuzekwa , Mnara wa tanki upo mita 6 na Tanki la chini linaendelea kufunikwa, Nyangamara- Nyumba ya Mtambo inaendelea kuezekwa, tanki la chini usawa wa kufunikwa na Mnara wa tanki umefikia | 78 | 2,382,106,380.81 | Ujenzi unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | mita 5.8, Nahukahuka- Mnara wa tanki umefikia mita 4.8. Pia amejenga vilula 21. Anaendelea na uchimbaji wa mitaro na ulazaji wa mabomba. | | | |
| Lindi DC | Mradi wa Maji Hingawali | 3500 | Kujenga matanki ya maji,kulaza bomba na kujenga vilula vya kuchotea maji | Mradi umekamilka | 100 | Mradi upo katika majaribio | Mradi upo katika majaribio |
| LINDI MC | Mradi wa Maji Kineng'ene | 3876 | Kununua na kusimika mtambo na jenereta katika kisima cha maji (12m3), Kujenga tanki la maji (100m3), Kujenga kibanda cha pampu, kuchimba na kulaza bomba, kujenga vituo 10 vya kuchotea maji, kujenga mifumo ya maji ya mvua, kufanya majaibio ya mradi (water testing) | Mradi umekamilika | 100 | 325,609,976 | Unatoa huduma |
| LINDI MC | Mradi wa Maji Tulieni | 2456 | Kununua na kusimika mtambo na jenereta katika kisima cha maji (9m3), Kujenga tanki la maji (50m3), Kujenga kibanda cha pampu, kuchimba na kulaza bomba, kujenga vituo 4 | Mradi umekamilika | 100 | 254,564,442.89 | Unatoa huduma |
| LINDI MC | Mradi wa | 5941 | Kununua na kusimika mtambo na | Mradi umekamilika | 100 | 500,795,963 | Kutokana na tatizo la |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Maji Kitumbikwela | | jenereta katika kisima cha maji (9m3), Kujenga tanki la maji (50m3), Kujenga kibanda cha pampu, kuchimba na kulaza bomba, kujenga vituo 4 vya kuchotea maji, kujenga mifumo ya maji ya mvua, kufanya majaibio ya mradi (water testing) | | | | pampu katika kisima cha Sinde, LUWASA hawajaanza kuingiza maji kwa hiyo mradi hautumiki kwa sasa. |
| LINDI MC | Mradi wa Maji Mtange | 2164 | Kununua mitambo na jenereta na kusimika katika kisima cha maji (7m3), Kujenga tanki la maji (15m3), Kujenga kibanda cha pampu, kuchimba na kulaza bomba, kujenga vituo | Mradi umekamilika | 100 | 187,037,684.71 | Unatoa huduma |
| LINDI MC | Mradi wa Maji Likotwa | 2929 | Kufanya extension ya mradi kutoka Mamlaka ya Maji (LUWASA):- Kujenga Sump, Kujenga kibanda cha pampu, Kununua na kusimika mtambo na jenereta, Kujenga tanki (50M3), Kuchimba na kulaza bomba, Kujenga vituo 7 vya kuchotea maji, kujenga mifumo ya maji ya mvua na kufanya majaibio ya mradi (water testing) | Mradi umekamilika | 100 | 366,906,464 | LUWASA hawajweza kuingiza maji |
| LINDI MC | Mradi wa Maji Mingoyo | 9888 | Kujenga kisima cha maji (28m3), Kujenga tanki la maji (135m3), Kujenga kibanda cha pampu, kuchimba na kulaza bomba, kujenga vituo 18 vya kuchotea | Mradi umekamilika | 100 | 667,190,696 | Unatoa huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaik a | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | maji, kujenga mifumo ya maji ya mvua na kufanya majaibio ya mradi (water testing) | | | | |
| LINDI MC | Mradi wa Maji Chikonji | 7000 | Kununua na kusimika mitambo ya kuvuta na kusukuma maji katika visima (35m^3 na 18m^3). kujengea vyanzo vya maji yaani 'Boreholes'. kujenga matanki matatu ya ujanzo tofauti 150m^3, 75m^3 na 25m^3. kuchimba mitaro na kulaza bomba. kujenga vituo 36 vya kuchotea maji. kujenga mifumo ya kuvunia maji ya mvua | Kununua mitambo ya kuvuta na kusukuma maji katika visima (35m^3 na 18m^3). kujengea vyanzo vya maji yaani 'Boreholes'. kujenga matanki matatu ya ujanzo tofauti 150m^3, 75m^3 na 25m^3. kuchimba mitaro na kulaza bomba. kujenga vituo 36 vya kuchotea maji. kujenga mifumo ya kuvunia maji ya mvua | 90 | 1,970,901,548 | Ujenzi unaendelea unatarajiwa kukamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2017 |
| LIWALE DC | Barikiwa | 5393 | ujenzi wa tenki umekamilika, nyumba ya mashine imekamilika, Ferrocement tenki 2 na tenki la plastic kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua umekamilika, generetana pampu | Mradi umekamilika | 100 | 374554110.7 | Unatoa huduma |
| LIWALE DC | Mpigamit i | 2665 | ujenzi wa tenki umekamilika, nyumba ya mashine imekamilika, | Mradi umekamilika | 100 | 296,662,300 | Unatoa huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaik a | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | Ferrocement tenki 2 na tenki la plastic kwa ajili ya uvunaji wa maji ya mvua umekamilika, generetana pampu zimefungwa tayari | | | | |
| LIWALE DC | Namihu | 1022 | Ujenzi wa Tanki, Nyumba ya mashine na Uvunaji wa maji ya mvua na ulazaji wa bomba mita 10241.5 | Mradi umekamilika | 100 | 322,054,555 | Unatoa huduma |
| LIWALE DC | Nabuya | 500 | Ujenzi wa mnara wa tenki la plastic mita 3, ulazaji wa bomba la raising main mita 600 na ujenzi wa kilula kimoja | Mradi umekamilika | 100 | 69,430,570 | Unatoa huduma |
| LIWALE DC | Kichonda , Mbaya and Namtumb wa | 4000 | ulazaji wa bomba mita 13000, ukarabati wa tenki la maji na ujenzi wa vilula . | Mradi umekamilika | 100 | 435,537,050.00 | Unatoa huduma |
| LIWALE DC | Namakol olo and Mitawa | 4000 | ulazaji wa bomba mita 10000 na ujenzi wa vilula vya kuchotea maji. | Mradi umekamilika | 100 | 381,830,000 | Unatoa huduma |
| NACHING WEA DC | Mkoka | 2120 | Kujenga nyumba ya mashine na uzio, Kujenga tanki la mita za ujazo 25, Kujenga vituo 8 vya kuchotea maji, Kufunga bomba kuu na kufukia mtaro umbali wa kilomita 1.4 na kilomita 4.808 kwa bomba la kusambaziai, kununua na kufunga pampu na Generata. | Mradi umekamilika | 100 | 280,466,068 | Unatoa huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaik a | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| NACHING WEA DC | Mituguru | 1250 | Kujenga nyumba ya mashine. Kujenga tanki la mita za ujazo 10, kufunga bomba kuu urefu wa kilomita 0.198 na bomba la usambazaji kilomita 3.45 | Mradi umekamilika | 100 | 175,294,953.3 | Kisima kinahitaji kusafishwa tena upya. |
| NACHING WEA DC | Chiola | 1980 | Kujenga nyumba ya mashine, Kujenga tanki la mita za ujazo 25, kulaza bomba kuu urefu wa kilomita 2.2, kulaza bomba la kusambazia maji urefu wa kilomita 3.849, Kujenga vituo 8 vya kuchotea maji, Kufunga Generata na pampu ya kusukuma Maji na Kujenga mfumo wa mfano wa uvunaji maji ya mvua | Mradi umekamilika | 100 | 280,466,068. | Unatoa huduma. |
| NACHING WEA DC | Lipuyu | 593 | Kujenga nyumba ya mashine, Kujenga tanki la ujazo wa lita 25,000, kufunga mabomba urefu wa mita za upandishaji Maji tankini, Kujenga vilula 3, Kufunga Generata na pampu ya kusukuma Maji na Kujenga mfumo wa mfano wa uvunaji maji ya mvua | Mradi umekamilika | 100 | 318,392,806.6 | Unatoa huduma |
| NACHING WEA DC | Nampem ba | 1920 | Kujenga nyumba ya mashine, Kujenga tanki la ujazo wa lita | Mradi umekamilika | 100 | 412,817,075 | Unatoa huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanaonufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | 25000, kufunga mabomba urefu wa mita 1815 za upandishaji Maji tankini, na mita 2382 bomba la usambazaji Kujenga vilula 4, Kufunga Generata na pampu ya kusukuma Maji na Kujenga mfumo wa mfano wa uvunaji maji ya mvua | | | | |
| NACHING WEA DC | Farm 8 | 761 | Ujenzi wa kitako cha pampu na Ufungaji wa pampu ya mkono(INDIA MARK II) Katika kisima kirefu kimoja, Ujenzi wa mifumo ya mfano ya uvunaji wa maji ya mvua | Mradi umekamilika | 100 | 24,458,930 | Unatoa huduma |
| NACHING WEA DC | Rweje | 1841 | Ujenzi wa kitako cha pampu na Ufungaji wa pampu ya mkono(INDIA MARK II) Katika kisima kirefu kimoja, Ujenzi wa mifumo ya mfano ya uvunaji wa maji ya mvua | Mradi umekamilika | 100 | 24,458,930 | Unatoa huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanaonufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| RUANGWA DC | Mradi wa Maji Luchelegwa | 2705 | Ujenzi wa<br>• Nyumba za mashine 1<br>• Mtandao wa Mabomba mita 3,338<br>• Tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa Lita 25,000<br>• Vituo vya kuchotea maji (DP) 9<br>• Ununuzi na Ufungaji wa Pampu za Maji na Genereta (KVA 9)<br>• Mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua wa mfano Mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua wa mfano wenye Matenki ya ujazo wa lita 1,000 5,000 na Simtank lita 3,000) | Mradi umekamilika | 100 | 207,027,430.50 | Unatoa huduma |
| RUANGWA DC | Mradi wa Maji Mbekenyera - Naunambe | 7249 | • Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba mita 9,154<br>• Ujenzi wa Tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa Lita 100,000<br>•Ujenzi wa Tenki la chini (Sump well) lenye ujazo wa Lita 25,000<br>• Ujenzi wa Nyumba za mashine 2<br>•Ujenzi wa Vituo vya kuchotea maji (DP) 20<br>•Uunganishaji wa Umeme (TANESCO Connection)<br>• Ununuzi na Ufungaji wa Chujio la Maji (Reverse Osmosis Plant)<br>• Ujenzi wa Mfumo wa uvunaji wa | • Ujenzi wa Nyumba za mashine 2 upo hatua ya rangi<br>• Ujenzi wa Vituo vya kuchotea maji (DP) pamoja chemba za mita za maji 24 umekamilika.<br>• Ujenzi wa tenki la kuhifadhia maji umekamilika<br>•Ujenzi wa mtandao wa bomba umekamilika | 95 | 737,643,270 | Ujenzi unaendelea, utakamilika mwishoni mwa mwezi Juni, 2017 |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaik a | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | maji ya mvua wa mfano yenye ujazo wa lita 1,000 na 5,000 na Simtank lita 3,000) Vijiji vya Mbekenyera na Naunambe | | | | |
| RUANGW A DC | Mradi wa Maji Ng'au - Nandagal a | 8654 | • Ujenzi wa Tegeo (Weir) • Ujenzi wa Matenki ya kuhifadhia maji 2 yenye ujazo wa Lita 50,000 kila moja • Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba mita 12,539 • Ujenzi wa Vituo vya kuchotea maji (DP) 22 • Ujenzi wa matenki (Ferrocement tanks) ya uvunaji wa maji ya mvua ya mfano yenye ujazo wa lita 1,000 na 5,000 | Mradi umekamilika | 100 | 659,786,710 | Unatoa huduma |
| RUANGW A DC | Mradi wa Maji Muungan o wa Mandawa | 12,243 | •Ujenzi wa Vituo vya kuchotea maji (DP) 45 •Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba mita 50,831 • Ujenzi wa Matenki matatu ya kuhifadhia maji yenye ujazo wa Lita 50,000 75,000 na 150,000 • Ujenzi wa Tegeo (Weir) • Ujenzi wa matenki | Mradi umekamilika | 100 | 1,296,513,527 | Unatoa huduma |

| MSM | Jina la Mradi | Idadi ya Watu wanao nufaika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Hali ya Utekelezaji | Asilimia ya Utekelezaji | Gharama za Mradi | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | (Ferrocement tanks) ya uvunaji wa maji ya mvua ya mfano yenye ujazo wa lita 1,000 , 3,000 na 5,000 | | | | |
| RUANGWA DC | Mradi wa Maji Mihewe | 1383 | • Ujenzi wa Mtandao wa Mabomba mita 3,285<br>• Ujenzi wa Tenki la kuhifadhia maji lenye ujazo wa Lita 25,000<br>• Ujenzi wa Tenki la chini (Sump well) ujazo wa Lita 25,000<br>• Ujenzi wa Nyumba za mashine 1<br>• Ujenzi wa Vituo vya kuchotea maji (DP) 5<br>• Ununuzi na Ufungaji wa Pampu na Generetor (39KVA)<br>• Ununuzi na Ufungaji wa Chujio la Maji (Reverse Osmosis Plant)<br>• Ujenzi wa matenki (Ferrocement tanks) ya uvunaji wa maji ya mvua ya mfano yenye ujazo wa lita 1,000 na 5,000 | Mradi umekamilka | 100 | 466,696,359 | Unatoa huduma |

## 1.3. Ujenzi wa Miradi Mingine ya Maji Vijijini

Katika mwaka 2016/2017, Serikali ya Mkoa imepanga kuendelea na juhudi nyingine mbalimbali za ujenzi wa miradi ya maji vijijini. Juhudi hizo ni zile zinazofanyika kupitia vyanzo mbalimbali vya fedha. Vyanzo hivyo ni pamoja na Halmashauri, Ruzuku ya Serikali kuu na Wadau mbalimbali waliopo katika Mkoa wetu na hata wa nje ya Mkoa. Juhudi hizo zinachangia katika kuinua kiwango cha upatikanaji wa huduma ya maji. **Jedwali Na. 5** linaonesha miradi ya maji itakayojengwa kwa ufadhili wa taasisi mbalimbali kutoka ndani na nje ya Mkoa

*Jedwali Na. 5:* **Miradi inayotekelezwa na Halmshauri pamoja na taasisi mbalimbali mwaka 2016/2017.**

| MSM | Taasisi/chanzo cha mapato | Mradi | | Gharama ( Shs) |
|---|---|---|---|---|
| | | Jina la Mradi | Hali ya utekelezaji (%) | |
| KILWA DC | SONGAS | Kinjumbi | 50 | 37,000,000 |
| RUANGWA DC | Ambassy of Japan in Tanzania (Grant assistance for Grass-roots Human Security Projects) | Ujenzi wa Mradi wa Maji Nangumbu | 80 | 173,585,406 |
| | | Ukarabati wa Mradi wa Maji Michenga | 70 | |

.

## 3.0. Hali ya huduma ya maji mji wa Lindi na miji mikuu ya wilaya

Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Mjini Lindi ina jukumu la kutoa huduma ya maji kwa wakazi wapatao 81,343 katika halmashauri ya Manispaa ya Lindi.

Hali ya huduma kwa kipindi hiki cha mwez Juni, 2017 ni ya kuridhisha kidogo, hii inatokana na kuongezeka kwa kisima kipya cha maji huko Sinde chenye uwezo wa uzalishaji wa mita za ujazo 55 kwa saa. Kwa maana hiyo changamoto ya upatikanaji wa maji kwa mgao kwa baadhi ya maeneo umepungua na kuna baadhi ya maeneo ambayo yalikuwa hayapati maji kwa sasa yameanza kupata huduma hiyo.

Kwa wastani tunazalisha na kusambaza mita za ujazo 2673 kwa siku ambapo ni asilimia 44.56 ya mahitaji halisi ya mita za ujazo 6000 kwa siku.

### A. Mpango wa Uboreshaji wa Huduma ya Maji katika Mji wa Lindi

Serikali imepata ufadhili kutoka Umoja wa Nchi za Ulaya kupitia *Millenium Development Goal Initiative* wa Euro Milioni 11.5 kwa ajili ya utekelezaji wa mradi wa majisafi na usafi wa mazingira katika manispaa ya Lindi. Mradi huu unatekelezwa kwa kushirikiana na serikali ya Ujerumani kupitia KfW (Benki ya Maendeleo ya Ujerumani).

Kazi zilizopangwa kufanyika ni: uchimbaji wa visima virefu 8; ujenzi wa chujio la maji lenye uwezo wa kusafisha maji mita za ujazo 7,500 kwa siku; ujenzi wa matanki mawili ya maji yenye ukubwa wa mita za ujazo 3,000 na 2000, ulazaji wa bomba kuu la maji umbali wa kilomita 11.5 na mabomba ya usambazaji maji umbali wa kilomita 27; ujenzi wa vituo 85 vya kuchota maji na ujenzi wa mabwawa ya kutibu majitaka na ununuzi wa gari la uondoshaji wa majitaka.

Mkataba wa ujenzi ulisainiwa kati ya Kampuni ya Overseas Infrastructure Alliance Pvt. Ltd ya India na Wizara ya Maji na Umwagiliaji tarehe 27 Machi, 2013. Muda wa Mkataba ulitakiwa kuisha tarehe 1 Desemba, 2015.

### B. Hatua iliyofikiwa

Uchimbaji wa visima 8 vyenye urefu wa mita 80 -120 vyenye uwezo wa kuzalisha mita za ujazo 7,500 kwa siku umekamilika na maji ya kutosha kukidhi mahitaji ya Manispaa ya Lindi

yamepatikana. Visima 5 kati ya 8 tayari vimefungwa pampu na visima 3 tayari vimeunganishwa na tanki la kuchuja maji. Visima 2 hivi sasa havifikiki kutokana na ubovu wa njia na kisima kimoja pampu yake iliibiwa na bado haijaletwa nyingine.
Matamki yote ya kuhifadhia maji na kusambaza maji yamekamilika, Maunganisho ya tanki na bomba la kupandisha maji yamekamilika.
Hatua zote za kuhakikisha maji yanafika mjini kabla ya tarehe 3/07/2017 zinaendelea vizuri, ukiondoa tatizo la kuunganisha umeme katika mitambo suala ambalo linaendelea kushughulikiwa na TANESCO.
Pamoja na kuwa kazi nyingine zitakuwa zinaendelea kukamilishwa, Maji yanatarajiwa kuanza kutoka katika mabomba kabla ya tarehe 3/07/2017.
Wizara imemwelekeza Mkandarasi kufanya kazi za kipaumbele ambazo zitawezesha kufikisha maji kwenye matanki.
Vilevile Wizara ilimwelekeza mhandisi mshauri GKW kuandaa gharama kwa ajili ya kupeleka maji kwa wananchi wa Ng'apa na Mitwero. Kwa upande wa Ng'apa Makisio ya awali yamefanyika ambapo jumla ya gharama ni Euro milioni 1.1m na kuhusu kupeleka Maji Mitwero gharama ni Euro milioni 2.788.

## 3.1 Hali ya Huduma za Maji Katika Miji Mikuu ya Wilaya

### 3.1.1 Mji wa Ruangwa

Mji wa Ruangwa una wakazi wapatao 13,577 kwa mujibu wa takwimu za Sensa ya watu na makazi ya mwaka 2012. Wakazi wanaopata huduma ya majisafi ni 7,763 sawa na asilimia 55 ya wakaazi wote waishio kwenye eneo hilo na huduma ya maji hupatikana kwa wastani wa masaa 4 kwa mgao wa siku 2 hadi 3. Vyanzo vya maji vinavyotumika ni visima virefu viwili (2) vilivyopo kwenye bonde la Matyatya. Uzalishaji wa maji ni mita za ujazo 348 kwa siku ukilinganisha na mahitaji ya mita za ujazo 1280 kwa siku.

**A. Mpango wa Uboreshaji kwa mwaka 2015/2016**

Wizara ya Maji na Umwagiliaji kwa kushirikiana na wadau mbalimbali wa Maendeleo, wamepanga kuufanyia ukarabati mkubwa Mradi wa maji Ruangwa mjini. Mwaka wa fedha 2015/2016 Wizara ya Maji ilitenga fedha jumla ya Tsh. 300,000,000 kwa ajili ya miradi yenye matokeo ya haraka (Quickwins). Fedha zilizopokelewa kutoka Wizara ya Maji na Umwagiliaji kipindi cha taarifa ni Tsh. 200,000,000/= Fedha hizi zimetumika kufanya kazi zifuatazo:kwa ajili ya kutekeleza baadhi ya kazi kwenye mradi tajwa kama ifuatavyo:-

i. Kufanya topographical survey eneo litakaloongezwa mtandao na eneo lote la mji lenye mtandao ili kuwa na ramani ya mtandao (digital map in A1 & A3 papers),
ii. Ununuzi wa viungo na viungio vya ukubwa mbalimbali ya usambazaji maji
iii. Ununuzi wa dira kwa ajili ya wateja wasio na dira pamoja na dira kubwa za kwenye mtandao na vyanzo vya maji na
iv. Ununuzi wa pampu

Katika mwaka huu wa fedha 2016/2017 Serikali imetoa fedha Shs. 400,000,000 ambazo zitatumika kufanya yafuatayo:-

i. Kujenga Tanki lenye ujazo wa lita 1,500,000
ii. Kununua na kufunga Dira za Maji kwa wateja 200

iii. Ununuzi wa mabomba ya kusambaza maji (4.14Km)

Mkataba na Mkandarasi umesainiwa mwezi mei, 2017 na hivi sasa Mkandarasi anafanya maandalizi ya kuanza kazi.

### 3.1.2 Mji wa Kilwa Masoko

Mamlaka ya Maji Kilwa Masoko ina wakazi **18,602** kwa mujibu wa takwimu za sensa ya Taifa iliyofanyika mwaka 2012. Wakazi wanaopata huduma ya majisafi ni **11,533** sawa na asilimia **62** ya wakazi wote. Mahitaji ya maji ni mita za ujazo **2270** kwa siku wakati Kiwango cha uzalishaji wa

maji ni mita za ujazo 1568 kwa siku endapo mitambo itafanya kazi kwa viwango vyake.Kutokana na matatizo ya umeme wastani wa uzalishaji ni 1064 kwa siku. Kiwango cha upotevu wa maji ni asilimia **24**

**A. Miradi inayoendelea Kujengwa**

Kipindi cha **2015/2016** Mamlaka ilipata Tsh **100,000,000** kwa ajili ya ukarabati wa mradi wa Maji Kilwa Masoko fedha ambazo zimewezesha kuchimba kisima kimoja, kununua bomba za ugawaji na kununua pampu ya kusukuma maji na kuongeza uzalishaji kutoka mita za ujazo **1360** kwa siku hadi **1568** kwa siku na kuongeza urefu wa mtandao wa Maji kutoka Km 43.9 hadi kufikia Km 48.5
Katika mwaka huu wa 2016/2017, Mamlaka ya Maji Kilwa Masoko imetengewa fedha Tshs 1,000,000,000 kwa ajili ya kuboresha huduma za maji Mjini Kilwa Masoko ili kufanya kazi zifuatazo:-

i. Kuchimba kisima eneo la Mpara
ii. Kujenga bomba la maji kutoka Mpara hadi Mihina
iii. Kujenga tanki la kuhifadhia maji lenye mita za ujazo 150 juu ya Mnara.

Mchakato wa Manunuzi ya Mkandarasi umekamilika na mkataba utasainiwa tarehe 21/07/2017.
Ipo changamoto ya ulipaji wa fidia kwa wananchi ambao maeneo yao yatatwaliwa wakati wa ujenzi wa mradi huu. Tathmini ya mara ya tatu imefanywa na Ofisi ya Bonde la Mto Ruvuma na Pwani ya Kusini na imekamilika. Wizara wameahidi kulipa fidia hiyo katika mwaka wa fedha 2017/18.

### 3.1.3 Mji wa Liwale

Mji wa Liwale una wakazi wapatao **31,448** kwa mujibu wa takwimu za sensa ya taifa iliyofanyika mwaka 2012. Wakazi wanaopata huduma ya majisafi ni **13,331** sawa na asilimia **42.39** ya wakazi wote waishio kwenye eneo hilo na huduma ya maji hupatikana kwa wastani wa **masaa 3**. vyanzo vya maji vinavyotumika ni mto Liwale pekee. Uzalishaji wa maji ni **mita za ujazo 864** kwa siku ukilinganisha na mahitaji ya **mita za ujazo 2,201.36** kwa siku. Upotevu wa maji **asilimia 42.2**.

### 3.1.4 Mji wa Nachingwea

Mahitaji ya maji kwa wakazi wa Nachingwea Mjini yanakadiriwa kuwa na wastani wa mita za ujazo 4,848.8 kwa siku. Wakati uzalishaji ni wastani wa mita za ujazo 2000 kwa siku kulingana na mtandao wa usambazaji uliopo. Hata hivyo uwezo wa chanzo cha maji cha Mbwinji ni kuzalisha mita za ujazo 13,651.2. Hali hii inaonesha haja kubwa ya kupanua mtandao wa usambazaji kwa mji wa Nachingwea na kuongeza vijiji vingine vilivyo karibu na mradi huu.
Mradi wa maji Nachingwea unaendeshwa na Mamlaka ya Maji Nachingwea- Masasi (MANAWASA). Kwa mji wa Nachingwea mradi umefikisha huduma kwa wakazi 49,471 kati ya wakazi 69,268 sawa na asilimia 71.41 ya wakazi wote wa mji huo. Mradi pia umefikisha huduma kwa wakazi 7,749 waliopo katika vijiji vya Likwachu na Chinongwe ambavyo vipo katika Wilaya ya Ruangwa. Vijiji hivi vimepitiwa na bomba kuu la maji liendalo katika mji wa Nachingwea. Lengo la Mamlaka ya Maji na Usafi wa Mazingira ya Masasi – Nachingwea (MANAWASA) ni kupeleka maji katika vijiji vyote vilivyopo Kilometa 5 kutoka bomba kuu.

Kwa wastani hali ya upatikanaji wa huduma ya maji kwa maeneo ya mijini ni asilimia 56.96%